# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA FEDHA

# CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI

**UDAHILI WA KOZI ZA ASTASHAHADA YA MSINGI (BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE) KWA MKUPUO WA SEPTEMBA KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026.**

Mkuu wa Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (Institute of Rural Development Planning) anawapongeza wanafunzi wote waliochanguliwa kujiunga katika kozi mbalimbali na kuwakaribisha wahitimu wote wa kidato cha nne wenye sifa ya kujiunga na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

Unaweza kutuma maombi mkupuo wa **SEPTEMBA** moja kwa moja chuoni kwa njia ya mtandao kupitia oas.irdp.ac.tz

**Kozi zitolewazo zinapatikana kwa ngazi ya Astashahada ya Msingi (Basic Technician Certificate) ni:**

i. Astashahada ya Mipango ya Maendeleo Vijijini (Basic Technician Certificate in Rural Development Planning).
ii. Astashahada ya Utawala na Usimamizi wa Maendeleo (Basic Technician Certificate in Development Administration and Management).
iii. Astashahada ya Maendeleo ya Jamii (Basic Technician Certificate in Community Development)
iv. Astashahada ya Msingi ya Upimaji Ardhi na Ramani (Basic Technician Certificate in Geomatics)
v. Astashahada ya Msingi ya Mipango Miji na Vijiji (Basic Technician Certificate in Urban and Regional Planning)
vi. Astashahada ya Msingi ya Uhasibu na Fedha (Basic Technician Certificate in Accounting and Finance)
vii. Astashahada ya Msingi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Basic Technician Certificate in Information and Communication Technology)
viii. Astashahada ya msingi katika Usimamizi wa Ardhi na Uthamini (Basic Technician Certificate in Land Management and Valuation)
ix. Astashahada ya Msingi katika Takwimu (Basic Technician Certificate in Statistics)
x. Astashahada ya Msingi katika Uchumi (Basic Technician Certificate in Economics)
xi. Astashahada ya Msingi katika Sheria (Basic Technician Certificate in Law)

**Sifa za Mwombaji:**
Mwombaji awe amehitimu **KIDATO CHA NNE** na kufaulu walau kwa kiwango cha alama “D” nne katika masomo yoyote isipokuwa somo la dini. Kwa waombaji wa astashahada ya Upimaji Ardhi na Ramani wanatakiwa kuwa na ufaulu wa walau kwa kiwango cha alama “D” kwa somo la Jiografia na Hisabati au Fizikia.

**Muda wa Masomo:**
Masomo ya Astashahada hutolewa kwa muda wa mwaka mmoja kwa mjumuisho wa mafunzo ya nadharia na vitendo.

**Kuripoti Chuoni**
Wanafunzi watapaswa kuripoti Chuoni **OKTOBA,** 2025 na kuwasili na vitu vifuatavyo: -

1. **Vyeti vya masomo**
Mwanafunzi wanapaswa kuwasili na vyeti halisi (original certificates) vya Taaluma na cha kuzaliwa (Zingatia: Chuo kitapokea nakala halisi ya matokeo "valid results slip" kwa waliomaliza 2024 tu)

2. **Ada**
Kwa wanafunzi wa kozi za Astashahada (Basic Technician Certificate, NTA Level 4) wakiwemo wale waliochaguliwa na serikali ada yao ni Sh. 940,000/= katika kozi zote isipokuwa kozi ya Astashahada ya Msingi ya Upimaji Ardhi (Geomatics), Astashahada ya Msingi ya Mipango Miji na Vijiji (Urban and Regional Planning) na Astashahada ya msingi katika Usimamizi wa Ardhi na Uthamini (Land Management and Valuation) ada yao ni Sh. 1,015,000/= inayolipwa kwa mchanganuo ufuatao;

**Jedwali Na. 1:** Mchanganuo wa ada kwa kozi za Astashahada ya Msingi (Basic Technician Certificate)

| | Siku ya Kuripoti | Baada ya Miezi Miwili | Jumla |
|---|---|---|---|
| Muhula wa Kwanza | Sh. 325,000 | Sh. 200,000 | Sh. 525,000 |
| Muhula wa Pili | Sh. 215,000 | Sh. 200,000 | Sh. 415,000 |
| Jumla Kuu | | | Sh. 940,000 |

**Jedwali Na. 2:** Mchanganuo wa ada kwa kozi za Astashahada ya Msingi ya Upimaji Ardhi (Geomatics), Mipango Miji na Vijiji (Urban and Regional Planning) na Astashahada ya msingi katika Usimamizi wa Ardhi na Uthamini (Land Management and Valuation)

| | Siku ya Kuripoti | Baada ya Miezi Miwili | Jumla |
|---|---|---|---|
| Muhula wa Kwanza | Sh. 355,000 | Sh. 205,000 | Sh. 560,000 |
| Muhula wa Pili | Sh. 235,000 | Sh. 220,000 | Sh. 455,000 |
| Jumla Kuu | | | Sh. 1,015,000 |

3. **Mahitaji mengine**
   i. Bima ya afya Sh. 50,400/= au Kadi ya bima ya afya ya NHIF inayofanya kazi
   ii. Gharama ya Mafunzo kwa Vitendo Sh.40,000/=
   iii. Gharama ya maombi ya kujiunga Sh. 10,000/=
   iv. Gharama ya vipimo vya afya Sh. 5000/= (Vipimo vinafanyika kwenye Zahanati ya Chuo)
   v. Gharama ya hosteli Sh. 350,000/= kwa Mwaka.
4. Malipo yote yatafanyika kwa **CONTROL NUMBER** zitakazotolewa kwenye mfumo wakati wa usajili
5. Wanafunzi watajigharamia gharama za chakula, shajala (stationary) na mafunzo ya vitendo
6. Chuoni hakuna sare, ila wanafunzi wanapaswa kuvaa mavazi yanayokubalika kwa mujibu wa miongozo na taratibu za serikali.

**Kwa msaada na maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi:**
Kampasi kuu Dodoma: 0746 777 001, 0746 777 002, 0746 777 003, 0746 777 004, 0746 777 006, 0746 888 063, 0746 888 064, AU 0744 254305
**Limetolewa Na:**
**Kurugenzi ya Huduma Saidizi za Taaluma**
**Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini**